



Lisa Van Thiel  
Early Childhood Coordinator  
(Mratibu wa Utoto wa Awali)  
978-674-2051  
[lvanthiel@lowell.k12.ma.us](mailto:lvanthiel@lowell.k12.ma.us)

**LOWELL PUBLIC SCHOOLS**  
*Ofisi za Usimamizi wa Kati Henry J. Mroz*  
155 Merrimack Street  
Lowell, Massachusetts 01852

## TIA MAKINI

# WAZAZI WA SHULE YA KIBINAFSI/WATOTO WA KUFUNZWA NYUMBANI

### Utambuzi kwa Mtoto

Ni wajibu wa Lowell Public Schools kutambua mtoto wowote ambaye anaweza kuwa na ulemavu ambaye ni mkaazi wa Lowell au ambaye huhudhuria shule ya kibinafsi ilio katika mipaka ya kijografia ya Lowell hata kama mtoto si mkaazi wa Lowell. Hii pia inawajumuisha wanafunzi ambao hufunzwa kwao nyumbani.

Lowell Public Schools pia ina wajibu wa kuwatathmini wanafunzi hao kuamua iwapo wanastahiki huduma za elimu maalum ama hudumu husika zilizo chini ya sheria ya serikali Shirikisho, IDEA (Kanuni ya Elimu kwa Watu binafsi walio na Malemavu) au, Sheria ya Jimbo la Massachusetts, 603 CMR 28 (Massachusetts Special Education Regulations (Kanuni za Elimu Maalum za Massachusetts)).

Lowell Public Schools pia inajitolea kuwatambua watoto kabla ya mwaka wao wa tatu wa kuzaliwa ili kutoa huduma za kuingilia kati za mapema kwa watoto walio na umri wa miaka mitatu na minne ambao wako na malemavu. Iwapo una maswali au wasiwasni kuhusu ukuaji wa mtoto wako na ungependa afanyiwe kipimo, tafadhali kamilisha Ombi la Kipimo cha Ukuaji kwa mtandao. Vipimo hufanyika kwa miadi pekee. Pindi unapokamilisha fomu la mtandao na kulitura, mmoja wa wafanyakazi wa Idara ya Utoto wa Awali atawasiliana nawe kufuatilia ombi lako na kukupangia miadi. Ukiwa na maswali yeoyote, tafadhali wasiliana na Idara ya Utoto wa Awali ukitumia nambari 978-674-2050.

Iwapo unashuku kwamba mtoto wako anaweza kuhitaji tathmini ili kuamua ustahiki wake wa huduma za elimu maalum, unaweza kuomba tathmini, kwa bure, kupitia Ofisi ya Elimu Maalum ya Lowell Public Schools. Tafadhali wasilisha ombi lako kwa [LPSSpedReferrals@lowell.k12.ma.us](mailto:LPSSpedReferrals@lowell.k12.ma.us). Iwapo una maswali kuhusu mchakato wa tathmini, tafadhali wasiliana na Idara ya Elimu Maalum, 155 Merrimack Street, 5<sup>th</sup> Floor, Lowell, MA au pigia 978-674-4322.

*Ilani hii imetolewa ikifuata sheria za Jimbo na Serikali Shirikisho kwa kutekeleza shughuli za Utambuzi kwa Mtoto ili kutambua wanafunzi ambao wanaweza kuwa na mahitaji ya tathmini ili kuamua ustahiki kwa huduma za elimu maalum.*